

GUSTAV NEUHAUS: MWALIMU WA KISWAHILI, MHARIRI NA MTUMISHI WA SERIKALI YA KIKOLONI¹

KATRIN BROMBER

Dibaji

Watumishi wa Taasisi ya Mambo ya Kiafrika ya Chuo Kikuu cha Humboldt walipotayarisha kuhama kwa taasisi yao kutoka Reinhardtstrasse mwaka 1995, boksi la jivu ilipatikana ndani ya kabati la chuma. Ndani yake zilihifadhiwa nyaraka za Kiswahili na Kiarabu zilizoandikwa kwa hati za Kiarabu. Kufuatana na lugha na maelezo yalioyoongezwa nyaraka hizo zilitoka Afrika Mashariki na kukusanywa na Gustav Neuhaus mwishoni mwa karne iliyopita.

Mwaka 1993 Ernst Dammann na wenzake walitoa katalogi yao ya nyaraka za lugha za Kiafrika. Ndani yake mtu hupata vilevile maelezo juu ya sehemu ya kwanza ya mkusanyo wa Neuhaus ambao unahifadhiwa katika Idara ya Nyaraka ya Maktaba inayoitwa Preussischer Kulturbesitz mjini Berlin (Dammann 1993: 79-80; 130-164). Baada ya kuzilinganisha nyaraka zilizotokea taasisi, mwaka 1995 na zile zilizokuwepo maktabani ilikuwa wazi kwamba nyaraka zilizogunduliwa si nakala. Sehemu hiyo ilipata alama ya rejista Hs. or. 10527 na kujumuisha nyaraka 161, 95 miongoni mwao ni za Kiarabu.

Lengo la makala hii ni yafuatayo: Kwanza, kutoa maelezo machache juu ya maisha ya Gustav Neuhaus kwani yeye ni mfano mzuri wa kuonyesha kwa namna gani watu waliofundishwa pale ili wafanye kazi ya kutawala ya kikoloni walivyovutiwa na lugha, fasihi na utamaduni. Mpaka sasa, hasa mchango wa wamisionari kama Karl Röhl au Johann Ludwig Krapf ulitiliwa mkazo tu. Pili, kuzungumzia matoleo yake ili kufafanua mchango wake katika masomo ya Kiswahili mjini Berlin na katika kupanua ujuzi juu ya lugha na utamaduni wa Waswahili. Tatu, kutumia mada ya utumwa kama ilivyoenezwa katika nyaraka mbalimbali za mkusanyo wa Neuhaus ili kuonyesha umuhimu wa nyaraka hizo kwa historia ya Afrika Mashariki. Zaidi ya hayo nyaraka hizo ni mifano mizuri ya Kimrimu kilivyotumiwa katika mawasiliano rasmi mwishoni mwa karne iliyopita.

Maisha wa Gustav Neuhaus na masomo yake katika Taasisi ya Lugha za Mashariki

Kuhusu kuzaliwa kwake tarehe mbili tofauti zinajulikana. Kwanza, Neuhaus alieleza katika dibaji ya *Kitabu Mauludi* (Neuhaus 1935: 150), kwamba alimpelekea mhariri mswada wake tarehe 11 Oktoba 1931, yaani siku ya kutimiza miaka 65 tangu kuzaliwa kwake. Maana yake alizaliwa mwaka 1866. Pili, tarehe 9 Juni mwaka 1902 Ali bin Nasir bin Sulaiman el-Lemki aliyekuwa liwali wa Dar es Salaam wakati huo alimtumia Neuhaus risala ya kumtakia kila la heri kwa sikukuu yake ya kuzaliwa (Hs. 10527, uk. 33). Vilevile, el-Lemki aliwasalimu mke na mtoto wake. Neuhaus alitaja jina la mke wake, Pia Augusta, katika dibaji ya *Kitabu*

¹ Ninawashukuru Sauda Barwani-Sheikh na Abdulatif Abdallah kwa kusahihisha Kiswahili changu

Mauludi. Bibi huyu alikufa mwaka 1931, wiki chache kabla ya kumaliza mswada huo. Hivyo, Neuhaus aliutabaruku kwa mke wake.

Kufuatana na maelezo yake yanayopatikana katika dibaji ya *Kitabu Mauludi* alijiandikisha katika Chuo Kikuu cha Berlin mwaka 1888 ili kusoma sheria. Wakati huo huo rafiki mmoja alimpa motisha kujifunza Kiswahili na baadaye Kiarabu katika Taasisi ya Lugha za Mashariki. Mwalimu wake wa Kiswahili alikuwa Carl Gotthilf Büttner aliyekuwa mwalimu wa kwanza wa Kiswahili katika Tasisi ya Lugha za Mashariki. Yeye alimfundisha kusoma Kiswahili kilichoandikwa kwa hati za Kiarabu, na zaidi ya hayo, alimpa moyo kushughulikia nyaraka hizo mwenyewe. Mwaka 1892 Neuhaus alihudhuria Mkutano wa Tisa wa Taaluma ya Lugha na Utamaduni wa Asia na Afrika Kaskazini uliofanyika mjini London. Akamaliza masomo yake mwaka huohuo.

Baada ya kuitishwa kwa huduma katika makoloni ya Ujerumani, mwaka 1893, alifanya kazi ya ukalimani ofisini mwa Freiheir von Soden aliyekuwa Gavana wa Afrika Mashariki, sehemu ya Ujerumani. Halafu akawa Mkuu wa Mkoa wa Pangani na hatimaye wa Mkoa wa Dar es Salaam. Wakati huo alianza kukusanya nyaraka za Kiswahili ambazo leo ziko katika Idara ya Nyaraka ya Maktaba inayoitwa Preussischer Kulturbesitz mjini Berlin.

Baada ya kurudi kutoka Afrika Mashariki Neuhaus alishinda mitihani ya kupata hadhi ya udaktari wa sheria. Hata hivyo, moyo wake ulitamani kushughulikia Kiswahili. Hivyo alikubali kwa furaha ombi la Taasisi ya Lugha za Mashariki kufundisha Kiswahili, kwa sababu Carl Gotthilf Büttner alikuwa amefariki mwaka 1892. Kuanzia mwaka 1895 mpaka 1900 Gustav Neuhaus alifundisha Kiswahili na kutoa mihadhara juu ya *Biashara na Njia za Mawasiliano katika Afrika Mashariki* na juu ya *Historia, Utawala na Sheria katika Koloni ya Deutsch-Ostafrika* (Verzeichnis der Vorlesungen an der Kaiser-Wilhelm-Universität zu Berlin, Jg. 1895-1900). Zaidi ya hayo aliratibu na kuongoza *Kongamano la Historia ya Makoloni ya Ujerumani katika Bara la Afrika* lililofanyika kila Jumamosi. Pia alisaidia kuhariri jarida la Taasisi, yaani *Mitteilungen des Seminars für Orientalische Sprachen*. Lakini Neuhaus hakuajiriwa kwa kudumu. Hakuna hati ya kumwajiri katika Nyaraka Kuu ya Chuo Kikuu ya Humboldt. Johannes Aasen aliyekusanya majina ya walimu wote waliofanya kazi katika Chuo Kikuu hicho alimtaja kama „Lektor für Swahili“ (Aasen 1955: 139). Maana ya „Lektor“ ni kulipwa vipindi vya masomo tu bila ya kuajiriwa.

Kazi yake inazidi ile ya kufundisha. Kitabu chake *Suahelimanuscripte in photolithographirten Originalen* (1896) ambamo alichapisha picha za nyaraka za Kiswahili pamoja na maelezo mafupi, kilikuwa msingi wa kufundisha Kiswahili kilichoandikwa katika hati za Kiarabu. Mwaka 1898 tafsiri yake inayoeleza matunda mbalimbali yaotayo Unguja ilitolewa katika jarida la taasisi (Neuhaus 1898).

Mwaka 1900, baada ya kumaliza muda wake mjini Berlin, Gustav Neuhaus alirejea Afrika Mashariki tena. Kule alipata hadhi ya Mkuu wa Mkoa wa Pangani na halafu alikuwa hakimu mkuu wa Tanga na hatimaye hakimu mkuu wa Dar es Salaam. Mwaka 1908 alipata matatizo ya afya na akarudi Ujerumani.

Mpaka sasa hayajulikani mengi juu ya maisha yake baada ya kurudi kutoka Afrika Mashariki. Mwaka 1935 tafsiri yake ya *Kitabu Mauludi* ilitolewa katika jarida la Taasisi ya Lugha za Mashariki. Neuhaus alitayarisha mswada huo pamoja na Martin Heepe, aliyefundisha Kiswahili, Yaunde, Duala na Herero na fonetiki katika taasisi wakati huo.

Mwaka 1931/32, baada ya kifo cha mke wake, alisafiri Afrika Mashariki tena. Alieleza safari hiyo katika kitabu chake cha mwisho kilichoitwa: *Suaheliland, wie ich es wiederfand. Eine Landreise von Kairo nach der Zanzibar-Küste in sieben Briefen* (Nchi ya Wasuaheli niliyoiona tena. Safari ya nchi kavu kutoka Kairo mpaka Unguja imeelezwa katika barua saba) (Neuhaus 1933). Miaka ya mwisho wa maisha yake bado yamo gizani. Hata terehe ya kifo chake haijulikani.

Matoleo ya Gustav Neuhaus

Nyaraka zote zilizohaririwa na kutafsiriwa na Gustav Neuhaus zilitungwa mwishoni mwa karne iliyopita. Waandishi walitumia hati za Kiarabu tu. Isipokuwa lugha ya *Kitabu cha Maulidi*, kilichotungwa nusu Kiamu nusu Kiarabu, zote nyingine ziliandikwa kwa Kimrima.

Kitabu chake alichandika kwa ajili ya masomo yake, yaani *Swahilimanuskripte in photolithographirten Originalen* (1896), ni mkusanyo wa nyaraka binafsi na rasmi, yaani barua na matangazo, maelezo juu ya desturi za kumzika mtu, na maandishi juu ya hukumu ya Sultani Seyyid Khalifa na watu wa mataifa mengine. Kinyume cha Carl Gotthilf Büttner, aliyetoa nyaraka za Kiswahili zilizopigwa chapa (Büttner 1892), Gustav Neuhaus alitumia nyaraka zilizopigwa picha yaani wanafunzi walilazimika kusoma hati za mkono. Vilevile, Neuhaus hakutoa tafsiri zao lakini aliongeza maelezo machache tu.

Maana ya kitabu hicho kwa utafiti wa historia na lugha itakuwa wazi tukiangalia kwa mfano maandishi juu ya hukumu ya Sultani Khalifa na watu wa mataifa mengine (Neuhaus 1896: 25-39 na picha 39). Kwa kusoma mtu hupata maelezo mazuri ya kihistoria juu ya mambo ya kisheria wakati wa Seyyid Khalifa. Zaidi ya hayo maandishi yenyewe yanaonyesha namna Kiswahili kilivyotumiwa katika maandishi eneo hili wakati huu. Mwandishi alianza kwa kuwagawa watu vikundivikundi. Kikundi cha kwanza ni Waarabu, Washihiri, Mabulushi na Wangazija, yaani „watu ambao wanajidai kwamba wao ni Muslimina“, na Waswahili (picha 3). Watu wa kikundi hicho huhukumiwa na Sultani. Kikundi cha pili, kilichohukumiwa kufuatana na sheria za kiingereza kilijumuisha Waingereza, Wahindi, Mabaniani ambao si Waislamu pamoja na watumwa walioachwa huru nao. Wafaransa na wakaazi wa makoloni yao walikuwa chini ya hukumu ya Wafaransa. Wajerumani, Wamarekani na Wareno walihukumiwa kufuatana na sheria za nchi zao. Watu wa kikundi cha mwisho waliitwa washenzi. Kwa maneno ya mwandishi, „asili yao na fasili yao [ni] Afrika“ (picha 3) Mwandishi aliendelea kwa kuunganisha swala la hukumu na swala la biashara ya utumwa kwa kueleza kwamba watu waliofanya biashara hiyo mara nyingi hukodi bendera ya kifaransa ili kuzuia Waingereza wasipande vyombo vyao (picha 3-5). Maelezo mengine yanahusu kesi mbalimbali na mahali na wakati ambapo hukumu hufanyika.

Kwa jumla hati ya mkono ya mwandishi huyu ni nzuri. Alihitilafiana fonimu za midomo /b/ na /p/ na fonimu ya midomo-meno /f/ na /v/ kwa kutumia herufi za kiarabu[ba:] na [fa:] yenye nukta tatu; sawa sawa na hati ya kiajemi. Kimorpholojia, mwandishi alitumia mtindo wa urejeshaji mara mbili, kama unavyoonyeshwa katika mfano wa kwanza:

Watu ambao wanaopenda kazi ya utumwa [...]

Jina la mwandishi hakutajwa hata mara moja. Kutokana na maoni yangu maelezo juu ya hukumu yaliandikwa na Sulaiman bin Said bin Ahmad Essorami aliyefundisha Kiswahili kuanzia mwaka 1891 hadi mwaka 1900 (Forstreuter et al. 1993: 40). Barua na mkusanyo wa mashairi wa Sulaiman bin Said vimo katika Idara ya Nyaraka ya Maktaba inayoitwa Preussischer Kulturbesitz mjini Berlin (Hs. or. 10527, k. 69, 86, 103, 116, 117, 126, 148).

Pia, ndiye mwandishi wa maelezo juu ya matunda yaotayo Unguja, yaliyotafsiriwa na kutolewa na Neuhaus katika jarida la taasisi mwaka 1898. Kinyume cha kitabu chake maandishi ya Kiswahili yalipigwa chapa na msomaji hana taabu kabisa kuisoma. Nyaraka zenyewe zinahifadhiwa katika Idara ya Nyaraka ya Maktaba Preussischer Kulturbesitz (Hs. or. 698). Katika aya ishirini Sulaiman bin Said anaeleza umbo, rangi, ladha na kutumia kwa matunda mbalimbali kama embe, chungwa, ndimu nk.

Sawa na maandishi juu ya hukumu mwandishi alitumia herufi maalum kwa fonimu midomo na midomo-meno zinazokosa sauti. Kuhusika kwa majina ya matunda kwa ngeli fulani kunabadilika mara kwa mara. Umoja wa embe, kwa mfano, unahusika na ngeli ya tano, lakini wingi wake unahusika na ngeli ya kumi, kama mfano wa pili unavyoonyesha (Neuhaus 1898: 123):

Aidha embe dogo kubwa / Aidha ziko embe buru rangi nyeupe, fahamu.

Kimorfolojia, mwandishi alitumia kiashi rejeshi kinachoshikilia *ku-*, yaani alama ya kitenzi kisoukomo. Tazama mfano wa tatu (Neuhaus 1898: 124):

Aidha tunda linalo kuitwa chungwa fahamu kwamba halipikwi huliwa bichi [...]

Sababu ya kushikilia kwake ingekuwa mwanzo wa kitenzi chenyewe, yaani kinaanza kwa irabu Gudrun Miehe alieleza kwamba mtindo huo wa kiashi ulitokea mara nyingi katika lugha ya utungo wa zamani (Miehe 1979: 175). Vitenzi vinavyoeleza utumiaji wa matunda vinaonyesha hali mazoea. Kawaida ya hati za Kiarabu ni kuandika bila ya alama ya kugawa au kumaliza. Mwandishi alionyesha mwanzo wa wazo au sentensi mpya kwa kutumia neno la *aidha*. Mwisho wa wazo fulani hudokezwa kwa kutumia msembo ya kiarabu *Mungu anajua*. Sawa na utungo mwingine kama tenzi, maandishi yana elementi ya utendaji ili kuunda uhusiano baina ya mwandishi na msomaji au msikilizaji. Tazama mfano wa nne (Neuhaus 1898: 123):

Aidha katika sura ya embe dodo fahamu kuna rangi yake moja kimanjano.

Neuhaus mwenyewe aliandika maandishi hayo katika hati ya Kirumi na kuyatafsiri kwa Kijerumani. Kwa bahati mbaya, alitolea tafsiri yaku tu bila ya kuongeza hata neno moja juu ya Kiswahili kilivyotumiwa na mwandishi.

Kazi yake ya mwisho katika fani ya Kiswahili ilikuwa toleo la *Kitabu Mauludi* katika jarida la Taasisi ya Lugha za Mashariki mwaka 1935 (Neuhaus 1935: 145-201). Kitabu kimetungwa kwa Kiarabu na Zain al-Abidin kutoka Barzanj. Sharifu Mansabu bin Sharifu Abdurahmani al-Hussaini aliyetoka Lamu na aliyefundishwa na Zain al-Abidi alikitafsiri kotoka Kiarabu kwa Kiswahili baada ya kuwasiliana na Carl Büttner. Kufuatana na maelezo

ya Neuhaus ndiye Büttner aliyetaka kukichapisha. Neuhaus aligundua kitabu hicho katika urithi wa Gustav Denhardt. Denhardt, aliyeishi muda mrefu Witu, alikuwa amefariki mwaka 1929.

Kitabu kinaanza kwa kueleza namna ya kusoma vizuri Maulidi. Kinaendelea kwa kutaja majina ya Mwenyezi Mungu tisini na tisa. Dua ya Kiarabu inatangulia Maulidi yenyewe. Nyaraka ya Kitabu cha Maulidi zinahifadhiwa katika Idara ya Nyaraka ya Maktaba inayoitwa Preussischer Kulturbesitz na kupata alama ya rejista Ms. or. Quart. 2025. Maelezo mafupi yanapatikana katika katalogi ya Ernst Dammann (Dammann 1993: 79).

Katika toleo lake Gustav Neuhaus alinakili na kutafsiri sehemu zilizotafsiriwa na Sharifu Mansabu. Bwana Björkman alinakili na kutafsiri sehemu zilizoandikwa kwa Kiarabu, yaani maandishi ya Ga'far al-Barzanj na utungo wa Zain al Abidi al-Barzanji.

Mkusanyo wa Gustav Neuhaus

Iliyoelezwa mwanzoni mwa makala haya, mkusanyo wa Gustav Neuhaus una sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inajumuisha nyaraka 117 zilizoelezwa katika katalogi ya Ernst Dammann.

Nyaraka 111 ziliandikwa kwa lugha ya Kiswahili ama katika hati za Kiarabu au za Kilatini na sita zimetungwa kwa Kiarabu. Nyaraka nyingi ni barua rasmi zilizotumiwa kwa Mkuu wa Mkoa wa Pangani. Aidha mtu anaweza kusoma mashairi kutoka Lamu, Mombasa na Pate. Tungo hizo zilitolewa na Ernst Dammann (Dammann 1940/41: 173-177). Nyaraka sita za Kiarabu ni matangazo manne ya Sultani Sayyid Khalifa pamoja na idhini mbili. Vilevile, sehemu hiyo ya mkusanyo unajumuisha maelezo juu ya ndoa na elimunyota na namna ya kuandika hati za Kiarabu na *Hekaya ya punda na ngombe kwa mtu mpandaji* (Hs. or. 1592-53).

Sehemu ya pili ya mkusanyo wa Neuhaus, ambayo haikuingizwa katika katalogi ya Ernst Dammann kwa sababu iligunduliwa baada ya kumaliza kwa katalogi hiyo inajumuisha nyaraka 161, 64 miongoni mwao ni za Kiswahili. Wingi wa nyaraka hizo ni barua rasmi na binafsi, stakabadhi, hati za deni na za arusi. Miongoni mwa nyaraka 64 za Kiswahili mbili ni ngano na moja ni utenzi. Kinyume cha nyaraka za sehemu ya kwanza nyingi zilikusanywa mjini Berlin. Neuhaus alizipata kutoka kwa Sulaiman bin Said bin Ahmed Eссорami na Amur bin Nasr el-Omeri yaani Waswahili wa kwanza waliofundisha Kiswahili katika Tasisi ya Lugha za Mashariki mwishoni mwa karne iliyopita.

Mada ya utumwa katika mkusanyo wa Neuhaus

Ili kufafanua umuhimu wa mkusanyo wa Gustav Neuhaus kwa utafiti wa historia ya eneo la Mrima nilichagua mada ya utumwa ilivyoelezwa katika buarua 14 ya sehemu ya kwanza ya mkusanyo huo.

Barua zote ziliandikwa kwa hati za Kiarabu na kutoka eneo la Pangani. Zinaonyesha mfumo wa kawaida, yaani huanza kwa kutaja jina la Mwenyezi Mungu na majina ya mtu anayeandikiwa barua. Mada ya barua hutangulia maelezo. Salamu na jina la mwandishi, pamoja na tarehe, humaliza barua hizo. Kwa jumla, lugha ya nyaraka hizo ni Kimrima. Barua zinaonyesha athari chache za lahaja nyingine za Kiswahili. Kwa kusoma barua hizo

niligundua matumizi ya kiambisho *ka-* ambacho kinawakilisha nafsi ya kwanza umoja wakati uliopo, na kiambisho *ta-* kinachowakilisha nafsi ya kwanza umoja wakati ufuatao. Mara nyingine waandishi hutumia kivumishi cha kumiliki nafsi ya tatu, yaani *yakwe*. Matumizi yote maatu hupatikana katika Kimvita au Kimtang'ata. Yanatokea hasa katika barua za Abdallah bin Hemedi 'I Ajemi, mwandishi wa *Habari ya Wakilindi* (Ajjemiy 1897), ambaye kufuatana na maelezo ya mwenzake Khalid Kirama, alikaa katika eneo hilo kwa muda.

Nilipoanza kusoma nyaraka hizo nilivutiwa sana na habari zake za historia. Tukisikia neno „utumwa“ umati wa watu wanaotiwa minyororo na kuteswa, hutokea mbele ya macho yetu. Lakini utumwa una sura nyingi, haswa Afrika Mashariki. Kuchungua sura hizo kumetiliwa mkazo hivi karibuni na wanahistoria kama Miers & Roberts (1988) na Deutsch (1996). Wanasema kwamba kuondoshwa kwa utumwa kulifanywa hatua kwa hatua. Mara nyingi mtumwa au kijakazi na bwana au bibi yake walipatana hali ya utumwa wa upande wa kwanza. Zaidi ya hayo, haina budi kutofautisha baina ya vitendo vya serikali mbalimbali za kikoloni. Wajerumani walifuata njia tofauti kulinganisha na Waingereza. Walitoa amri kadhaa ili kustawisha hali ya watumwa na vijakazi. Baina ya miaka 1890 na 1900 serikali ya kikoloni ilipiga marufuku kukamata watu wengi na kuwauza, lakini hawakukataza biashara ya watumwa kwa jumla. Ilichukua miaka mitano zaidi mpaka Wajerumani walipoamuru kwamba watoto wote waliozaliwa kuanzia tarehe 1 mwezi wa kwanza mwaka 1906 wawe watu huru (Landesgesetzgebung 1911: 331-332). Utumwa wa nyumbani haukukubaliwa tu na serikali ya kikoloni, bali ulirekebishwa nayo.

Na urekebishaji huo unajidhihirisha katika barua zilizokusanywa na Neuhaus. Vikundi viwili vilipata barua hizo: Kimoja kilikuwa wakuu wa serikali ya kikoloni wa mkoa, yaani *Bezirksamtänner* au mabwana wakubwa. Kingine kilikuwa Waafrika waliopewa hadhi ya uliwali au ujumbe. Lakini barua zinaonyesha wazi kwamba Majumbe au maliwali walisita kutoa amri yoyote iliyohusu swala la utumwa. Badala yake waliieleza serikali ya kikoloni habari zote zilizohusu kesi fulani na kuwaomba kufanya uamuzi. Mfano mzuri ni barua ya liwali Omari bin Stambuli aliyeomba ruhusa kwa niaba ya mtu mwingine kuwatafuta watumwa wawili ambao walitoroka (Hs. or. 772-47). Inawezekana kusema kwamba kesi zote za utumwa zilijadiliwa na kuamuliwa kufuatana na mfumo maalum.

Jambo lisilo la kawaida ni barua ya mwanamke kwa bwana mkubwa. Kore binti Kimiya alimwomba moja kwa moja kumwacha huru kwa muda kijakazi mja mzito ili asijifungue korokoroni. Zaidi ya hayo, alimweleza juu ya matatizo ya fedha yaliyotokea wakati wa kumnunua kijakazi huyo. Labda kuzungumzia swala la kike kulimpa haki Kore binti Kimiya kumwandikia moja kwa moja bila ya kujadili jambo hilo na liwali au jumbe kabla yake na kutumia mfumo wa kawaida wa kuwasiliana (Hs. or. 772-15.).

Kando ya kesi za kibinafsi zilizohusu kukamatwa kwa watumwa waliotoroka au biashara potevu au mauaji ya watumwa, waandishi wengine walitoa maoni yao juu ya maswala yaliyohusu watu wengi. Mgoma wa Bauro bin Mkafi Bauro, kwa mfano, alimweleza bwana mkubwa kwamba wapagazi kadhaa walimkimbia na hana haki kuwatafuta wala kuwalazimisha. Anajuta sana kutokuwa na watumwa kwa kazi ya upagazi. Kukatazwa kwa kuwawinda watu na biashara ya watumwa wengi kuliwataabisha haswa wale watu wa pwani waliofanya biashara ya masafa marefu bara (Hs. or. 2285-34).

Mfano mwingine ni barua ya Jumbe Abu Bakr Ali (Hs. or. 10527). Kwa niaba ya wazee alilalamika kwamba watumwa hucheza ngoma mpaka saa sita usiku na hawawezi kufanya kazi siku ifuatayo. Anaiomba serikali ya kikoloni kutatua tatizo hilo kwa kutoa amri ya kuwakataza watumwa wasishiriki katika ngoma. Kwa bahati mbaya hatujui jibu au kitendo cha serikali. Lakini masilahi za pande zote mbili zilikutana katika kesi hiyo. Kuanzia mwanzo wa ukoloni Wajerumani walikuwa macho sana kila watu walipocheza ngoma.

Kama nilivyosema mwanzoni, utawala wa Wajerumani ulibadilisha mfumo wa utumwa kwa kutoa amri zilizotajwa. Lakini tunajua kwamba kumwacha huru mtumwa au kijakazi si uvumbuzi wa kijerumani bali kumeshapendekezwa na Kurani. Serikali ya kikoloni ilihimiza na kufanya rasmi tu mwenendo huo. Baina ya miaka 1891 na 1912 iliidhinisha vyeti vya uhuru 52,300. Wengi waliopata uhuru hawakurudi bara tena. Walibaki Mrima. Tatizo lililotokea sasa lilikuwa swala la nafasi yao katika jamii. Je, uhuru wao uliwapa hadhi ya kiungwana au hadhi ya watumwa walioachwa huru tu? Sitaki kujadili swala la uungwana hapa. Lakini barua zinaonyesha kwamba waungwana wengine walikuwa macho sana ili kuwazuia watumwa au vijakazi wasipate hadhi hiyo bure. Nitoe mfano! Katika barua ya Mwinyi Mzee Kawamba Mshare bin Kawamba Saisi alieleza ugunduzi wake kwamba suriya wa Mwinyi min Tanga si mwungwana bali ni kijakazi. Ushahidi ni kwamba mama wa suriya wake alikuwa kijakazi na mtoto huyo si mtoto wa bwana wake bali baba ni mtumwa. Kwa hiyo Simba wa Mrima ana haki kumtendea kama kijakazi (Hs. or. 1592-2). Mfano mwingine unaeleza juu ya kijakazi aliyepata cheti chake cha uhuru Dar es Salaam na kukamatwa na Fundi Bilala huko karibu na Pangani. Baada ya kuchana cheti cha mwanamke huyo alimwaza kama kijakazi. Mnunuzi aliposikia habari ya kijakazi wake aliiomba serikali ya Pangani kutatua tatizo hilo. Walipiga simu Dar es Salaam na kupata nambari ya cheti cha uhuru kisichompa kijakazi huyo uhuru tu bali hadhi ya uungwana pia (Hs. or. 772-23). Mpaka sasa sijapata cho chote kinachoeleza maoni ya Wajerumani juu ya maana ya hadhi hiyo ya uungwana. Lakini walitumia neno hilo katika vyeti vya uhuru vilivyotolewa nao.

Kujadili maswala ya utumwa na kutatua matatizo rasmi kusidhihirishe kwamba serikali ya kikoloni ilirekebisha swala hilo tu bali ilitakiwa kuleta uwiano baina ya pande mbili zilizobishana. Wahusika wa kiafrika walitaka kuzuia wasilaumiwe. Zaidi ya hayo urasimu wa utumwa wa nyumbani ulilenga shabaha ya kuleta makubaliano baina ya serikali ya kikoloni na Waafrika waliokuwa na hadhi ya juu ambao wanahitajiwa na Wajerumani ili kumiliki Afrika Mashariki. Kukataza utumwa kwa jumla sawa na mfumo wa Waingereza kungalizusha mivutano mikali baina ya pande hizi mbili. Kutoupiga marufuku kuliwezesha utumwa uendelee mpaka mwisho wa ukoloni wa Wajerumani na athari yake ilihisika hata baada ya uhuru wa Tanzania.

Mwisho

Madhumuni ya makala hayo ilikuwa kuonyesha kwamba Gustav Neuhaus aliyepata masomo ya lugha na sheria ili afanye kazi ya utawala katika kolonia la Deutsch-Ostafrika alivutiwa na maisha na lugha na utamaduni wa Mrima. Hatimaye alianza kukusanya nyaraka na kuzitafsiri na kuzitoa. Nyaraka hizo zina umuhimu kwa isimu kwani tumepata mifano mizuri Kiswahili kilichotumiwa katika mawasiliano rasmi.

Maelezo juu ya utumwa yamelenga kufafanua umuhimu wa nyaraka hizo kwa kuelewa historia ya eneo hilo la Afrika Mashariki na kipengele kimoja cha historia ya utawala wa kikoloni wa Wajerumani. Pia zinasisitiza tena ushirikiano baina ya wanaisimu na wanahistoria katika kazi zao za utafiti.

Marejeo

- Aasen, J. 1955. *Gesamtverzeichnis der Lehrkörper der Universität Berlin*. Bd. I: 1810-1945. Leipzig.
- Ajjemiy, A. H. 1897. *Habari ya Wakilindi*. Magila.
- Dammann, E. 1993. *Afrikanische Handschriften. Teil 1: Handschriften in Swahili und anderen Sprachen Afrikas*. Stuttgart.
- Deutsch, J. G. 1996. Weidner's Slaves. A Misunderstanding in German Colonial Thought *Working Papers of the Institute of Development Studies* 4. [University of Helsinki].
- Forstreuter, B. et al. 1993. Zur Geschichte der Afrikanistik an der Berliner Universität/Humboldt-Universität. *Berliner Afrikanistische Arbeitsblätter* 1 (1993).
- Landes-Gesetzgebung. 1911. *Die Landes-Gesetzgebung des Ostafrikanischen Schutzgebietes Verordnung vom 24. Dezember 1904*. Tanga/Dar es Salaam. Uk. 331-332.
- Miehe, G. 1979. *Die Sprache der älteren Swahili-Dichtung (Phonologie und Morphologie)*. Berlin.
- Miers, S./ Roberts, R. (whr.) 1988. *The End of Slavery in Africa*. Madison.
- Neuhaus, G. 1896. *Suaheli-Manuskripte in photolithographirten Originalen*. Berlin.
- Neuhaus, G. 1898. Der Obstreichthum der Insel Zanzibar. *Mitteilungen des Seminars für Orientalische Sprachen* I (1898): 120-137.
- Neuhaus, G. 1933. *Suaheliland, wie ich es wiederfand Eine Landreise von Kairo nach der Zanzibarküste in sieben Briefen*. Stuttgart.
- Neuhaus, G. 1935. Kitabu Mauludi. Buch der Geburt Muhammed's. *Mitteilungen des Seminars für Orientalische Sprachen* XXXVIII: 145-201.